



The President of the
United Republic of
Tanzania

The State House
Dar es Salaam

14 Juni, 2016

Mwenyekiti,
Jumuiya ya Watanzania,
MAREKANI.

Yah: **SHUKRANI KWA WATANZANIA WAISHIO MAREKANI**

Natoa shukrani zangu za dhati kwako Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watanzania waishio Marekani na kupitia kwako, shukrani hizo pia ziwafikie watanzania wenzangu wote waishio Marekani kwa cheti cha shukrani mlichopatia Ofisi ya Rais kwa kuchangia mafanikio ya Kongamano la DICOTA na vile vile zawadi ya fulana mliyoniletea. Cheti hicho na fulana hiyo kwa hakika ni ukumbusho mzuri.

Nimefurahi sana kupata taarifa na kusoma kwenye mtandao wenu kuwa Kongamano la DICOTA mlilofanya kuanzia tarehe 28 Aprili hadi tarehe 1 Mei, 2016, lilifanyika kwa mafanikio makubwa. Ingawa sikuweza kuhudhuria, nimefurahi kuwa Balozi wetu wa Tanzania nchini Marekani, Mhe. Wilson W. Masilingi aliniwakilisha vyema katika kongamano hilo. Hivyo, ushirikiano mliouonyesha katika kongamano hilo ni vizuri mkauendeleza.

Aidha, nawaomba muendeleo kufanya kazi kwa bidii huko mliko na kama nilivyowahimiza katika hotuba iliyosomwa na Balozi kwa niaba yangu wakati wa Kongamano hilo, endeleeni kukumbuka nyumbani, Tanzania, kwa maendeleo binafsi, ngazi ya familia na Taifa kwa ujumla. Na kwa upande wangu, ninawahakikishia kuwa Serikali itaendelea kuwatambua na kuwashirikisha watanzania mnaoishi nje ya nchi mkiwa sehemu ya wadau muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Nchi ni yetu sote na ni kwa kushirikiana kwa pamoja tutaweza kuleta maendeleo ya Taifa letu la Tanzania.

Nawatakieni kila la kheri.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'John Pombe Joseph Magufuli'.

Dkt. John Pombe Joseph Magufuli
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA